EFF'S SURVEILLANCE SELF-DEFENSE

# NAMNA YA: KUSIMBA SIMU YAKO YA IPHONE

https://ssd.eff.org/en/about-surveillance-self-defense

ELECTRONIC FRONTIER FOUNDATION

LOCALIZATION LAB

Kusimba data kwenye simu yako ya iPhone si rahisi kama kuunda nenosiri. Kwa kuwa data yako nyingi pia huenda ikahifadhiwa mtandaoni, ni muhimu pia kuelewa jinsi hifadhi hiyo ya mtandaoni inavyofanya kazi, na kuzingatia kuwezesha kipengele cha ziada ambacho huilinda data hiyo vyema.

## Jinsi Data Inavyosimbwa kwenye Kifaa

Ikiwa una simu ya iPhone au kifaa cha iPad, unaweza kulinda taarifa za kifaa chako kwa kutumia usimbaji fiche. Hiyo ina maana kwamba ikiwa mtu atakipata kifaa chako, basi atahitaji pia nambari yako ya siri ili kusimbua kile kilichohifadhiwa humo, ikiwa ni pamoja na anwani, ujumbe wa papo hapo au jumbe fupi, rekodi za simu na barua pepe.

Vifaa vya kisasa vya Apple husimba kwa njia fiche taarifa kwa njia ya chaguomsingi, vikiwa na viwango mbalimbali vya ulinzi. Usimbaji fiche huo hulingana na toleo la simu uliyo nayo na hali ya simu yako (kama vile ikiwa imefungwa au imefunguliwa, au ikiwa imewashwa tu kutoka kwa hali ya kuzimwa.)

Ili kulinda kupatikana kwa data yako dhidi na mtu kwa kuiba kifaa chako, unahitaji kuunganisha usimbaji fiche huo na fungu nywila au msimbo unaoujua peke yako.

Kulingana na mwongozo wake wa walinda usalama, nambari ya siri ikiwa imewezeshwa, Apple haiwezi kusaidia watekelezaji wa sheria kuchomoa taarifa: "Kwa vifaa vyote vinavyotumia iOS 8.0 na matoleo ya hivi karibuni, Apple haiwezi kutoa data ya kifaa cha iOS kwa kuwa data inayotafutwa na wwalinda usalama imesimbwa kwa njia fiche na Apple haina ufunguo wa kusimbua data hiyo. iPhone 6 zote na miundo ya baadaye ya vifaa hutengenezwa kwa kutumia iOS 8.0 au toleo la baadaye la iOS. Hata hivyo, kumbuka kuwa baadhi ya idara za walinda usalama zinaweza kuwa na njia nyingine za kufikia data kwenye simu yako bila kuhitaji usaidizi wa Apple.

> Nchini Marekani, kutumia mfumo wa kibayometriki nchini Marekani—kama vile kuchanganua uso au alama ya vidole—kufungua simu yako kunaweza pia kuathiri ulinzi wa kisheria wa taarifa za simu yako uliyopewa chini ya ruhusa ya Marekebisho ya Tano dhidi ya kutiwa hatiani kwa lazima. Chini ya sheria ya sasa ya Marekani—ambayo bado inabadilikabadilika—kutumia nambari ya siri iliyohifadhiwa akilini kwa ujumla hutoa msingi thabiti wa kisheria wa kujisitiri dhidi ya amri ya mahakama ya kulazimishwa kufungua/kusimbua kifaa chako. Ingawa EFF inaendelea kupambana ili kuimarisha ulinzi wetu wa kisheria dhidi ya kulazimisha watu kusimbua vifaa vyao, kwa sasa kuna ulinzi mdogo dhidi ya

kulazimishwa kufungua kifaa kwa alama za vidole kuliko ilivyo dhidi ya ufichuzi wa nenosiri uliolazimishwa.

Huenda uliweka aina fulani ya nambari ya siri ulipopata simu yako ya iPhone kwa mara ya kwanza, lakini ikiwa ulichagua kutofanya hivyo, au ungependa kubadilisha jinsi ya kufungua kifaa chako, unaweza kufanya hivyo kwa kwenda kwenye ***Mipangilio*** > ***Kitambulisho cha Uso (au Mguso) na Nambari ya siri***. Hapa, unaweza kuweka mbinu ya kufungua au kuzima utumiaji wa kibayometriki kuingia kwa kifaa chako na kuweka nambari ya siri pekee. Unaweza kufanya hivyo kwa kutengua chaguo la "Kufungua iPhone" chini ya "Tumia Kitambulisho cha Uso (au Mguso)."

Ukipenda, unaweza pia kubadilisha nambari ya siri inayotumiwa na simu yako. Fungua ***Mipangilio*** > ***Kitambulisho cha Uso (au Mguso) na Nambari ya siri***na uguse "Badilisha Nambari ya siri" (itaonyesha "Weka Nambari ya siri" ikiwa hukuweka nambari ya siri ulipotayarisha simu yako kwa mara ya kwanza). Unapoombwa "Weka nambari yako mpya ya siri," gusa "Chaguo za Msimbo wa siri" na utapewa chaguo kati ya urefu tofauti wa nambari au msimbo (wa herufi pamoja na nambari).

Ikiwa kwa sababu yoyote unahitaji kuzuia kitambulisho cha Uso (au Mguso) kwa muda kisitumike kufunguasimu yako ya iPhone, unaweza kufanya hivyo bila kuingia kwenye menyu ya mipangilio:

Bonyeza na ushikilie kitufe cha kuwasha/kuzima kifaa na moja kati ya kitufe cha kuongeza au kupunguza sauti hadi chaguo la kuzima kitelezi/kupiga simu ya dharura lionekane (unaweza kufanya hivi ikiwa simu yako imefungwa au haijafungwa). Ukibofya "ghairi," simu yako sasa itahitaji nambari ya siri ili kuifungua.

## Jinsi Data ya iCloud Inavyosimbwa

Ikiwa unatumia kifaa cha Apple, kuna nafasi nzuri ya kuhifadhi angalau baadhi ya data kwenye huduma ya wingu ya Apple, ambayo inaitwa iCloud. Hii inaweza kujumuisha taarifa mbalimbali, kuanzia orodha yako ya wawasiliani na faili za programu hadi chelezo nzima ya iPhone yako. Baadhi ya data hii imesimbwa kwa njia fiche kutoka mwanzo hadi mwisho-kumaanisha ni wewe tu utakuwa na njia ya kuisimbua data, si Apple-kwa chaguo-msingi. Huku baadhi ya data inaweza kufikiwa na Apple.

Apple inarejelea kategoria zake za usimbaji wa iCloud kama "Ulinzi wa Kawaida wa Data," au "Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data." Kategoria ya Ulinzi wa Kawaida wa Data ni aina ya usimbaji fiche unaowezeshwa kwa chaguomsingi, huku Ulinzi wa Data wa Hali ya Juu ni kipengele ambacho utahitaji kuwasha kwa hiari.

## Maana ya "Ulinzi wa Kawaida wa Data"

Ulinzi wa Kawaida wa Data unamaanisha kuwa data nyingi iliyohifadhiwa katika iCloud huhifadhiwa kwa funguo za usimbaji fiche ambazo Apple inaweza kuzifikia. Vifunguo vya usimbaji fiche kutoka kwa vifaa vyako huhifadhiwa kwenye seva za Apple, kwa hiyo Apple inaweza kusimbua data hiyo inapohitajika. Hii inamaanisha kuwa kampuni pia inaweza kukusaidia kurejesha nenosiri lako ikiwa umelisahau. Hata kwa Usimbaji wa Kawaida wa Data, baadhi ya data husimbwa kwa njia fiche kutoka mwanzo hadi mwisho, ikijumuisha maelezo yanayoweza kuwa ya faragha kama vile data ya Jarida, data ya Afya, pasi za Wallet na manenosiri yoyote unayohifadhi kwenye kidhibiti cha nenosiri kilichojengewa ndani.

Hata hivyo, Usimbaji wa Kawaida wa Data hausimbi kwa njia fiche Chelezo ya iCloud ya kifaa chako au chelezo ya mazungumzo katika Arafa kutoka mwanzo hadi mwisho. Hii ina maana kwamba Apple inaweza kufikia ufunguo wa usimbaji fiche na kuweza kusimbua data ambayo huenda ni nyeti.

## Maana ya "Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data"

Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data huwezesha usimbaji fiche kutoka mwanzo hadi mwisho lakini Ulinzi wa Kawaida wa Data husimba data tu wakati unapitishwa kwenye seva za Apple. Hii inamanisha kuwa unaweza kudhibiti funguo za usimbaji fiche na Apple haitaweza kufikia data yoyote kati ya hizi. Inamaanisha pia kwamba Apple haitaweza kukusaidia kurejesha ufikiaji wa akaunti yako. Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data hujumuisha maelezo mengi muhimu, ikiwa ni pamoja na chelezo yako ya iCloud (ambayo inajumuisha chelezo ya Arafa), Hifadhi ya iCloud, picha, vidokezo, vikumbusho na maelezo zaidi katika jedwali lililo hapa chini.

Uwezeshaji wa Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data, husababisha chelezo zako na faili muhimu zaidi kupata manufaa ya usimbaji fiche kutoka mwanzo hadi mwisho, kulinda faili zako dhidi ya ufuatiliaji wa watu wengi, wafanyikazi walaghai wa Apple, au uwezekano wa kuvuja kwa data. Kumbuka kwamba Apple haiwezi kukusaidia kurejesha data hii ikiwa utapoteza ufikiaji wa akaunti yako, au vifaa vyovyote ambavyo funguo zimehifadhiwa. Ili kulinda dhidi ya hili, Apple hukuruhusu kuunda ufunguo wa urejeshi unaojihifadhi, au unaweza kukabidhi mwasiliani wa urejeshi, mtu anayeaminika ambaye anaweza kutoa msimbo ambao utakusaidia kurejesha ufikiaji wa akaunti yako. Mwasiliani wako wa urejeshi hawezi kufikia data yako yoyote ya iCloud.

Bado kuna baadhi ya aina za data ambazo hazijajumuishwa katika Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data. Mara nyingi hii ni data iliyosanidiwa kulingana na viwango vilivyokuwepo awali, ikiwa ni pamoja na Kalenda, Anwani, na iCloud Mail. Hizi zitaendelea kuhifadhiwa

na Ulinzi wa Kawaida wa Data. Kama ilivyobainishwa katika mwongozo wake wa utekelezaji wa sheria, Apple pia bado inakusanya baadhi ya metadata kuhusu chelezo, faili za Hifadhi ya iCloud, picha, vidokezo, alamisho na ujumbe.

Vile vile, si programu zote zinazotumia iCloud kulandanisha au kuhifadhi data zitawezeshwa na Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data. Huenda ukahitaji kuwasiliana na msanidi wa programu moja kwa moja ili upate ufafanuzi kuhusu jinsi programu inavyohifadhi data. Hili linaweza kuwa muhimu zaidi kujua kwa aina fulani za programu, kama vile vidokezo au programu ya kuandika majarida, kuliko zingine, kama vile programu ya kuhifadhi mapishi.

Ikiwa data itahifadhiwa kwa mfumo wa Ulinzi wa Hali ya Juu ya Data, basi vifaa vyako vinashikilia funguo za kusimbua data hiyo. Ikiwa imehifadhiwa kwa mfumo wa Ulinzi wa Kawaida wa Data, basi Apple hushikilia funguo. Hiyo inamaanisha kuwa kampuni hiyo ina uwezo wa kusimbua data hiyo yenyewe, na hata kujumuisha katika kujibu maombi kutoka kwa watekelezaji wa sheria.

## Je, data ya iCloud imesimbwa kwa njia fiche kutoka mwanzo hadi mwisho?

| | Ulinzi wa Kawaida wa Data | Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data |
|---|---|---|
| Miamala ya Kadi ya Apple | ✔️ | ✔️ |
| Kalenda | | |
| Wawasiliani | | |
| Muundo huria | | ✔️ |
| Data ya Kiafya | ✔️ | ✔️ |
| Data ya Nyumbani | ✔️ | ✔️ |
| Chelezo ya iCloud | | ✔️ |
| Hifadhi ya iCloud | | ✔️ |
| Baruapepe ya iCloud | | |
| Data ya Jarida | ✔️ | ✔️ |
| Ramani | ✔️ | ✔️ |

| | | |
|---|---|---|
| Memoji | ✔️ | ✔️ |
| Ujumbe kwenye iCloud | ✔️ | ✔️ |
| Vidokezo | | ✔️ |
| Manenosiri na Kishikilia kifunguo | ✔️ | ✔️ |
| Maelezo ya Malipo | ✔️ | ✔️ |
| Picha | | ✔️ |
| Msamiati Uliofunzwa wa Kibodi ya QuickType | ✔️ | ✔️ |
| Vikumbusho | | ✔️ |
| Safari | ✔️ | ✔️ |
| Alamisho za Safari | | ✔️ |
| Muda wa Matumizi wa Simu | ✔️ | ✔️ |
| Taarifa za Siri | ✔️ | ✔️ |
| Njia Mkato ya Siri | | ✔️ |
| Kumbukumbu za Sauti | | ✔️ |
| Funguo za Bluetooth za W1 na H1 | ✔️ | ✔️ |
| Pasi za Wallet | | ✔️ |
| Manenosiri ya Wi-Fi | ✔️ | ✔️ |

## Jinsi Data Inavyolindwa Wakati wa Kushiriki au Kushirikiana

Ikiwa unatumia zana zozote za ushirikiano za Apple kushiriki data na wengine, basi kuna mambo machache ya kuzingatia jinsi usimbaji fiche wa mwanzo hadi mwisho unavyofanya kazi.

Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data hutumiwa kwa taarifa zinavyoshirikiwa mradi tu zimeshirikiwa na mtu mwingine ambaye amewasha kipengele cha Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data. Ikiwa mna folda ya pamoja ya Hifadhi ya iCloud, Vidokezo vilivyoshirikiwa, au mnatumia Maktaba ya Picha Inayoshirikiwa ya iCloud, washiriki wote lazima

wawezeshe kipengele cha Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data ili uwezo wa kushiriki data uweze kufanya kazi. Kwa mfano, ikiwa una folda ya Hifadhi ya iCloud ambayo unashiriki na mtu fulani, na nyote mmewasha Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data, basi folda hiyo itasalia ikiwa imesimbwa kutoka mwanzo hadi mwisho. Hata hivyo, unaposhirika faili hakuna ishara ya kuonyesha kuwa mtu unayeshiriki naye amewasha Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data. Kwa hivyo, hakikisha kuwa umewasiliana na watu wengine kabla ya kushiriki nao faili muhimu.

Hata hivyo, ukitumia aina yoyote ya ushirikiano wa iWork, kama vile kufanya kazi na wengine kwenye waraka katika Kurasa au Nambari, faili hizo hazijasimbwa kwa njia fiche kutoka mwanzo hadi mwisho. Vile vile, ikiwa unashiriki faili au folda kwa kutumia chaguo la "ifikiwe na yeyote aliye na kiungo" kutoka kwa programu, kama vile Faili au Picha, basi hiyo haijasimbwa tena kutoka mwanzo hadi mwisho. Katika hali hizi, Ulinzi wa Kawaida wa Data hutumiwa.

## Namna ya Kuwezesha Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data

Unaweza kuwezesha Ulinzi wa Hali ya Juu ya Data kutoka kwa kifaa cha iPhone, iPad au Mac, na itatumika kwenye kila kifaa kingine cha Apple unachomiliki.

Lakini kabla ya kuiwasha, unahitaji kuchukua hatua kadhaa: [wezesha uthibitishaji wa vipengele viwili] kwa akaunti yako ya Apple ikiwa bado hujafanya hivyo, na usasishe vifaa vyako vyote vya Apple (angalau viwe na toleo la iOS 16.3, iPadOS 16.3, macOS 13.2). , tvOS 16.3, watchOS 9.3, ingawa unaweza kuhitajika kutumia sasisho la hivi majuzi zaidi), au jipya zaidi. Ikiwa una vifaa vya zamani vilivyounganishwa kwenye akaunti ya iCloud ambayo unawasha Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data, na haviwezi kusasishwa, zingatia kuwasha Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data kwa sasa. Tutazungumzia sababu na kutoa mbinu mbadala hapa chini. Ukiweza kusasisha, fuata hatua hizi ili kuwasha usimbaji fiche kutoka mwanzo hadi mwisho:

1. Kwenye kifaa cha iPhone au iPad, fungua ***Mipangilio*** (au ***Mipangilio ya Mfumo*** kwenye Mac) ***> "Jina lako"> iCloud > Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data > Urejeshaji wa Akaunti***. Utapewa chaguo mojawapo kati ya mbili za mbinu ya urejeshaji. Hii hukusaidia kurejesha ufikiaji wa akaunti yako kwa kuwa Apple haitaweza kukusaidia. Lazima uchague angalau njia moja ya urejeshaji, au unaweza kufanya zote mbili:
    a. **Mrejeshaji wa akaunti:** Huyu ni rafiki au mwanafamilia anayemiliki kifaa cha Apple na anayeweza kukusaidia kurejesha ufikiaji wa akaunti yako ikihitajika. Hawataweza kufikia data yako yoyote, lakini badala yake wataweza kukutumia msimbo wa urejeshi ambao utakurudisha ndani. Unaweza kuziondoa kwenye menyu hii siku zijazo, ukihitaji.

   b. **Ufunguo wa kurejesha akaunti**: Huu ni msimbo wa herufi 28 ambao hukurejesha kwenye akaunti yako ikihitajika. Apple haipati nakala, kwa hivyo ukiipoteza, unaweza kupoteza ufikiaji wa akaunti yako ya Apple kabisa. Ukichagua njia hii, utahitaji kuandika ufunguo mara kadhaa, kwa hivyo uandike.
2. Rudi kwenye ***Mipangilio*** (au ***Mipangilio ya Mfumo*** kwenye Mac) ***> "Jina lako"> Ulinzi wa Haki ya Juu wa Data ya iCloud > Menyu ya Urejeshaji wa Akaunti*** na uguse "**Washa Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data**" na ufuate vidokezo. Utahitaji kuweka Namba ya Utambulisho Binafsi ya simu yako na ufunguo wa kurejesha akaunti, ukichagua njia hiyo ya kurejesha uwezo wa kufikia akaunti.

Baada ya kuweka mipangilio ya Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data, hupaswi kuifikiria tena isipokuwa unapojaribu kutayarisha kifaa kipya ambacho ulinunua kikiwa na toleo la zamani la Mfumo wa Uendeshaji (katika hali ambayo huenda ukahitajika kuzima kwa muda Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data ). Au unahitaji kufanya urejeshaji wa akaunti, au unahitaji kufikia data yako ya iCloud kutoka kwa kivinjari. Ikiwa unafikia data mara kwa mara kutoka iCloud.com, nenda kwenye ***Mipangilio*** > ***"Jina lako"*** > ***iCloud*** na uguse **Fikia Data ya iCloud kwenye Wavuti *ili kuwasha ufikiaji ikiwa unaihitaji.***

Ikiwa una kifaa cha zamani ambacho hakiwezi kusasishwa kuwa iOS 16.3 au toleo jipya zaidi, uwezeshaji wa Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data unawezekana tu ikiwa utaondoa Kitambulisho chako cha Apple kwenye kifaa hicho. Katika hali nyingi, hii inafanya kifaa hicho kutokuwa na maana. Kwa mfano, ikiwa una Apple TV ya zamani ambayo haiwezi kusasishwa, kuiondoa hukuzuia kufikia Duka la Programu na Kitambulisho chako cha Apple, hukuzuia kutumia Netflix, Hulu, na programu zote nyingine. Apple inapaswa kurahisisha mchakato huu, na kuwapa watu chaguo la kujiandikisha kwa Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data bila kuondoa Kitambulisho cha Apple kwenye vifaa vya zamani. Hata kama hiyo inamaanisha kuondoa ufikiaji wa vipengele fulani vya kushiriki, kama vile hifadhi ya iCloud Drive au Apple Photos.

Kuna matumaini. Kwa baadhi ya vifaa, kama vile Apple TV au MacBook ya zamani, suluhisho la tatizo hili ni kuunda Kitambulisho cha pili cha Apple, kisha kukiweka kama mwanafamilia katika [Kushiriki kwa Familia](), ambayo inapaswa kujumuisha usajili wako mwingi au vipakuliwa vya Duka la Programu, lakini haitakipa kifaa hicho idhini ya kufikia aina ya data iliyojumuishwa katika Ulinzi wa Hali ya Juu wa Data. Kwa mfano, hutaweza kufikia maktaba yako ya picha, lakini bado unaweza kufikia usajili wa Netflix unaolipia kupitia Apple (ikiwa hautalipia usajili wowote kupitia Apple, hutakuwa na chochote cha kukupa wasiwasi. ) Huu unaweza kuwa [mchakato unaochosha kufanya](). Suluhu hii haitafanya kazi kwa kifaa kinachotegemea sana data iliyolandanishwa, kama Apple Watch.